NSW Health

# Chanjo kabla, wakati na baada ya ujauzito



Kupata chanjo ukiwa mjamzito ni muhimu. Chanjo husaidia mwili wako kutengeneza kingamwili zinazolinda wewe na mtoto wako. Kingamwili hizi hupewa mtoto wako kabla ya kuzaliwa, na kuwaweka salama katika miezi michache ya kwanza ya maisha.

Influenza (mafua), pertussis (kifaduro) na respiratory syncytial virus (virusi vya kupumua vya syncytial (RSV)) ni bila malipo kwa wanawake wajawazito.

## Chanjo za kupata kabla ya ujauzito

Baadhi ya chanjo ni bora kupata kabla ya kuwa mjamzito. Muulize daktari wako ikiwa unahitaji hizi:

- **Chanjo ya MMR:** Inalinda dhidi ya surua[1], mabusha (mumps)[2] na rubela[3].
- **Chanjo ya Varisela:** Hukinga dhidi ya tetekuwanga (chickenpox)[4].

## Je, chanjo ni salama wakati wa ujauzito?

Ndiyo, chanjo zinazopendekezwa wakati wa ujauzito ni salama kwako na kwa mtoto wako. Hulinda dhidi ya magonjwa makali kwa kupatia kingamwili zako mtoto wako kabla ya kuzaliwa.

Unaweza kupata chanjo kwa:

- daktari wa familia (GP) wako
- mtoa matunzo ya uzazi wako anayekushugulikia (km mkunga, daktari wa uzazi)
- mfamasia wako
- Huduma ya matibabu yako ya wa Aboriginal.

| Chanjo | Wakati gani | Gharama | Kwa nini Ni Muhimu |
|---|---|---|---|
| Mafua[5] (influenza) | Wakati wowote wa ujauzito | Bila malipo* | Influenza, au mafua, ni virusi vya kupumua ambavyo huenea kwa urahisi (kama vile kwa kukohoa na kupiga chafya) na huweza kusababisha homa, kikohozi, na uchovu.<br><br>Chanjo inakukinga na mafua makali na husaidia kuweka mtoto wako salama katika miezi 6 yake ya kwanza kwani yeye ni mchanga mno kupata chanjo yake ya mafua. Watoto walio chini ya umri wa miezi 6 wana uwezekano mkubwa wa kwenda hospitalini wakiwa na mafua kuliko watoto wakubwa. |
| Kifaduro[6] (pertussis) | 20-32 wiki (kawaida katika wiki 28) | Bila malipo* | Kifaduro (pertussis) ni ugonjwa unaoambukiza sana unaoenea kwa urahisi (kama vile kwa kukohoa na kupiga chafya). Unaweza kusababisha kikohozi kikali na unaweza kufanya iwe vigumu kupumua, hasa kwa watoto wachanga. Chanjo hulinda mtoto wako kutokana na kifaduro hadi aweze kupata chanjo yake mwenyewe akiwa na umri wa wiki 6.<br><br>Wale karibu zaidi na mtoto wako (kama vile mwenzi wako, ndugu au babu na nyanya wa mtoto wako) wanapaswa pia kupewa chanjo ikiwa hawajapata chanjo hiyo katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. |
| RSV[7] (Abrysvo) | 28 - wiki 36 (kawaida katika wiki 28) | Bila malipo* | RSV ni virusi ya kawaida ambayo huweza kusababisha mafua na matatizo ya kupumua, hasa kwa watoto wachanga na watoto wadogo.<br><br>Chanjo hulinda mtoto wako dhidi ya RSV wakati wa miezei yake 6 ya kwanza. Chanjo hii haihitajiki kwa walezi wengine. |

*Baadhi ya watoa huduma huenda wakalipishe ada ndogo kwa kutoa chanjo.
Uliza daktari, mkunga, au mfamasia wako.

[1] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/factsheets/Pages/measles_factsheet.aspx
[2] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/factsheets/Pages/mumps.aspx
[3] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/factsheets/Pages/rubella-german-measles.aspx
[4] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/factsheets/Pages/Chickenpox.aspx
[5] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/Influenza/Pages/default.aspx
[6] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/whoopingcough/Pages/default.aspx
[7] https://www.health.nsw.gov.au/Infectious/factsheets/Pages/respiratory-syncytial-virus.aspx

Chanjo ya COVID 19 si chanjo iliopendekezwa mara kwa mara wakati wa mimba lakini inapendekezwa kwa wajawazito ambao hawajachanjwa ili kupunguza hatari ya COVID-19 kali. Wanawake wajawazito ambao tayari wamechanjwa wanaweza kuzungumza kuhusu dozi zaidi na mtoaji wao wa huduma ya afya. Chanjo ya COVID-19 ni bila malipo* wakati wowote wakati wa ujauzito.

## Baada ya mtoto wako kuzaliwa

**Kwa ajili yako**

Chanjo nyingi ni salama kupata mara baada ya kujifungua, hata kama unanyonyesha. Ikiwa ulikosa chanjo ya kifaduro wakati wa ujauzito, pata kabla ya kuondoka hospitali.

Zungumza na daktari wako au mkunga kuhusu chanjo nyingine yoyote ambayo unaweza kuhitaji.

**Kwa mtoto wako**

Chanjo kwa wakati[8] ndiyo kinga bora ya mtoto wako dhidi ya magonjwa makali. Atapata chanjo ya hepatitis B mara tu baada ya kuzaliwa.

Chanjo zinazofuata za mtoto wako zitatolewa akiwa na umri wa wiki 6.

Baadhi ya watoto wanaweza kuhitaji chanjo ya RSV ya watoto wachanga (nirsevimab) ikiwa mama hakupata chanjo ya RSV au ikiwa mtoto yuko katika hatari kubwa ya kuugua sana kutokana na RSV. Uliza daktari wako au mkunga ikiwa hii inatumika kwa mtoto wako.

## Una swali?

Piga simu muuguzi wa afya ya mtoto kwa **1800 882 436** (7am hadi saa sita usiku, kila siku).

## Rasilimali za ziada

- Programu za kinga[9]
- Australian Immunisation Register (Usajili wa Kinga wa Australia)[10]
- NCIRS – Rasilimali na habari ya kinga[11]
- Idara ya Afya ya Jumuiya ya Madola na Utunzaji Wazee - Chanjo[12]
- AusVaxSafety[13]
- MotherSafe (MamaSalama)[14]
- SKAI[15]

*Baadhi ya watoa huduma huenda wakalipishe ada ndogo kwa kutoa chanjo. Uliza daktari, mkunga, au mfamasia wako.

[8] https://www.health.nsw.gov.au/vaccinate
[9] https://www.health.nsw.gov.au/immunisation/pages/default.aspx
[10] https://www.servicesaustralia.gov.au/individuals/services/medicare/australian-immunisation-register
[11] http://www.ncirs.org.au/
[12] https://www.health.gov.au/health-topics/immunisation
[13] https://ausvaxsafety.org.au/
[14] https://www.seslhd.health.nsw.gov.au/royal-hospital-for-women/services-clinics/directory/mothersafe
[15] https://skai.org.au/pregnancy-and-newborn

Tembelea **www.health.nsw.gov.au/pregnancy-vaccinations**



Februari 2025 © NSW Health. SHPN (HPNSW) 250108